



# Vituko vya wanyama



Tusome Early Literacy Programme


# Vituko vya wanyama



Mbuzi wa baba yangu yupo karibu na mlang'o.

Paka wa dada yangu yupo juu ya kabati.






Nguruwe wa kaka yangu yupo kwenye shimo la takataka.

Ng'ombe wa mjomba wangu wamo ndani ya zizi.





Kondoo na sungura wa binamu zangu wamechafua godoro.

Mbwa na punda wa babu yangu wameharibu maua.





Bata na kuku wa shangazi yangu wamevunja birika  
na bilauri zake.



Bata mzinga wa amu amepitia dirishani na kuchafua mkeka.

## Maswali

1. Mbuzi wa baba yupo wapi?
2. Nguruwe wa kaka yupo wapi?
3. Kondoo na sungura wamechafua nini?
4. Maua yameharibiwa na nani?
5. Birika na bilauri vimevunjwa na nani?

# Vituko vya wanyama

Kuanzia mbuzi wa baba hadi bata  
mzinga wa amu, kila mnyama  
nyumbani anafanya vituko tofauti.



Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka  
kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la  
Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo  
ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia  
mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.